**HOTUBA YA DKT. HASHIL T. ABDALLAH KATIBU MKUU WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA YA KUFUNGA KIKAO KAZI KATI BRELA NA TAASISI ZA UDHIBITI TAREHE 15 SEPTEMBA, 2023 MKOANI MOROGORO**

- **Bw. Godfrey Nyaissa Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA,**
- **Wakurugenzi na Watumishi wa BRELA,**
- **Maafisa Waandamizi kutoka Taasisi za Udhibiti**
- **Ndugu Waandishi wa Habari,**
- **Mabibi na Mabwana.**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

***Ndugu washiriki, mabibi na mabwana***

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuturuzuku uhai, afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa katika Kikao Kazi hiki kilichaandaliwa na BRELA kwa lengo la kuzikutanisha Taasisi na Mamlaka mbalimbali za udhibiti katika Sekta ya Biashara nchini. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru washiriki wote kwa kushiriki kikamilifu katika Kikao Kazi hiki ambacho mmeweza kujadili namna ya kuboresha utendaji

kazi ili kuboresha mazingira ya biashara na kukuza uwekezaji kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

***Ndugu washiriki, mabibi na mabwana***

Napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Bw. Godfrey Nyaisa, Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, kwa kunialika ili kujumuika nanyi kufunga Kikao Kazi hiki. Mimi kama kiongozi mwenye dhamana ya kusimamia Sekta ya Viwanda na Biashara nchini, nilipokea mwaliko huu kwa furaha na unyenyekevu mkubwa nikiwa na Imani kuwa yote mliyokubaliana na kuafikiana yatachangia kuleta matokeo chanya katika kukuza na kuendeleza Sekta ya biashara yenye mchango mkubwa katika kukuza ajira na uchumi wa nchi.

***Ndugu Washiriki mabibi na mabwana***

Ni matumaini yangu kuwa sote tunatambua jitihada zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa miongozo na maelekezo ya kufanya mageuzi ya Kisera, Kisheria na Kikanuni katika Taasisi na Mamlaka mbalimbali za udhibiti ili kuboresha na kukuza Sekta ya Biashara na uwekezaji. Katika kutimiza azma hiyo ya Mheshimiwa Rais, Wizara ya Viwanda na Biashara inatekeleza maono hayo kwa vitendo kwa kufanya mapitio ya Sera zake hususan Sera Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 ambayo kwa sasa iko katika ngazi ya Baraza la Mawaziri. Mapitio ya Sera hii yamezingatia wakati wa sasa wa ufanyaji biashara, mabadiliko ya sayansi na teknolojia pamoja na malengo ya Jumuiya mbalimbali za Kikanda na Kimataifa ambazo Tanzania imeridhia kuwa mwanachama.

***Ndugu Washiriki, Mabibi na mabwana***

Kwa upande wa Sheria na Kanuni, Wizara pamoja na Tasisi na Mamlaka za Udhibiti zimeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) ambapo Sheria mbalimbali za Taasisi zinazohusika na biashara zimefanyiwa marekebisho kwa kufuta au kurekebisha baadhi ya vifungu vilivyokuwa vinaleta mgongano katika utekelezaji hivyo kuwa kero kwa Wafanyabiashara. Kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 ambayo utekelezaji wake umeanza tarehe 01 Julai, 2023, jumla ya Sheria sitini na saba (67) zimefanyiwa marekebisho mbalimbali. Aidha, utekelezaji wa MKUMBI unaendelea ambapo Serikali imelenga kuondoa vikwazo vyote vya Kisera, Kisheria na Kikanuni ili kuweka urahisi wa uanzishaji na ufanyaji biashara nchini

***Ndugu Washiri, mabibi na mabwana***

Natambua pia kuwa maboresho ya mazingira ya kuanzisha na kufanya biashara nchini yanakwenda sambamba na uanzishwaji wa Mifumo ya Kielektroniki ambayo inasaidia kupunguza gharama za kuanzishaji na kufanya biashara kwa kuwawezesha wafanyabiashara kupata huduma hizo wakiwa mahali popote nchini bila kulazimika kuzifuata huduma hizo katika Ofisi za Serikali. Katika hili natambua juhudi madhubuti zilizochukuliwa na BRELA kwa kuwezesha huduma zake zote kutolewa kwa njia ya mtandao hali iliyochangia kwa kiasi kikubwa kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa Wakala pamoja na kupunguza vitendo vya rushwa kwa baadhi ya watumishi wasio waaminifu, kupunguza matumizi ya Vishoka ambao walikuwa wakilalamikiwa kuwaibia wafanyabiashara. Aidha, naomba kutoa rai kwa mamlaka nyingine za udhibiti kuiga mfano wa BRELA kwa kuhakikisha kuwa huduma zenu zote zinatolewa kwa njia ya kielektroniki.

***Ndugu washiriki, mabibi na mabwana***

Mageuzi hayo yanayofanywa na Serikali, yanalenga pia kuwawezesha wazalishaji wa bidhaa na wafanyabiashara wetu kuzifikia fursa mbalimbali za masoko ya Kikanda na Kimataifa ili kukuza mauzo ya nje na kuiwezesha nchi yetu kuongeza wigo wa ajira na fedha za kigeni. Kama sote tunavyofahamu, Serikali kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia Itifaki mbalimbali hususan Itifaki ya Soko Huru la Biashara Afrika (African Continent Free Trade Area - AfCFTA) ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kufungua fursa za masoko baina ya nchi za Afrika. Aidha, katika kutimiza azma hiyo, Wizara imeendelea kuchukua hatua madhubuti ikiwemo kuanzisha Mkakati wa Kukuza Mauzo ya Nje (Export Strategy) ambao uko katika hatua za mwisho kukamilika pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wadau ili kutambua fursa za AfCFTA.

***Ndugu Washiriki, mabibi na mabwana***

Ni matumaini yangu kuwa kuwepo kwenu hapa kwa muda wa siku tatu kumewapa fursa ya kujadiliana, kubadilishana uzoefu na kukubaliana njia bora za kuboresha utendaji kazi wenu ili kutimiza maono na dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kujenga taifa lenye uchumi imara kupitia sekta ya biashara. Aidha, naomba kuchukua nafasi hii kuwaomba mtakaporejea kwenye taasisi zenu kuwa chachu ya mabadiliko kwa kufanyia kazi yale yote mliyoazimia na kukubaliana katika kikao hiki. Ni vema sote tukatambua kuwa, utendaji wetu utapimwa na kuwa na tija kwa kulea na kukuza biashara badala ya kuwa chanzo cha kuua biashara.

***Ndugu Washiriki, mabibi na mabwana***

Kabla sijamalizia hotuba yangu, naomba kutumia fursa hii kuwahakikishia kuwa, Wizara yetu ambayo imepewa dhamana ya kusimamia sekta hii pamoja na Taasisi zilizo chini yake itaendelea kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoathiri uanzishwaji na ufanyaji wa biashara. Wizara kupitia taasisi zake itaendelea kukutana mara kwa mara na wadau wa Sekta hii hususan wafanyabiashara ili kupokea changamoto zao pamoja na kuwapatia mrejesho wa hatua mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali kuboresha sekta hii.

***Ndugu washiriki, mabibi na mabwana***

Baada ya kusema hayo, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwenu nyote kwa ushiriki wenu. Aidha, kwa namna ya pekee tuwapongeze na kuwashukuru BRELA kwa kuona umuhimu wa kuwa na kikao hiki cha pamoja kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na kukubaliana namna bora ya kutekeleza majukumu yenu.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza**

**Janhuri ya Muungano wa Tanzania……….**